



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA UUGUZI NA UKUNGA TANZANIA



TAARIFA KWA UMMA

KUSUDIO LA KUWAONDOA KWENYE DAFTARI LA USAJILI NA UORODHESHWAJI WAUGUZI NA WAKUNGA AMBAO HAWAJAHUISHA LESENI.

Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania ni mamlaka ya kisheria iliyoanzishwa kwa ajili ya kusimamia Wataaluma na Taaluma za Uuguzi na Ukunga ili kuulinda umma dhidi ya huduma zinazotolewa na Wauguzi na Wakunga nchini. Baraza linafanya kazi chini ya Sheria ya Uuguzi na Ukunga inayoitwa "**The Nursing and Midwifery Act, 2010**" na Kanuni zake.

Leseni za Uuguzi na Ukunga zipo kisheria kama ilivyoelekezwa katika **kifungu cha 21(1) na (2) na 38(1)** cha **Sheria ya Uuguzi na Ukunga Na. 1 ya mwaka 2010**. Zoezi la uhuishaji wa Leseni za Uuguzi na Ukunga kwa msimu husika hufunguliwa kila ifikapo tarehe 01 Julai na kukamilika tarehe 31 Disemba.

Baada ya kufanya tathimini ya zoezi hili imebainika kuwa kuna baadhi ya **Wauguzi na Wakunga** ambao hawajahuisha Leseni zao. Ofisi ya Msajili inakusudia kuwasilisha jambo hili katika kikao cha Baraza ili wale wote ambao hawajahuisha leseni zao na hawajatoa taarifa yoyote ofisi ya Msajili kumjulisha kwamba Wamestaafu, hawatoi huduma za Uuguzi na Ukunga au wamebadilisha taaluma n.k, waweze kutolewa/kufutwa kwenye daftari la Usajili/Uorodheshwaji kwa mujibu wa **kifungu cha 18 cha Sheria ya Uuguzi na Ukunga ya mwaka 2010** na Kanuni ya 8(b) ya Usajili, Uorodheshaji na Utoaji Leseni (**Registration, Enrollment and Licencing Regulation, 2010**).

Aidha, baada ya kuondolewa kwenye rejestra au orodha Muuguzi au Mkunga huyu hatoweza kurejeshwa kwenye daftari la Usajili kabla ya kutimiza miaka mitano (5) kuanzia tarehe aliyoondelewa kwa mujibwa wa Kanuni ya 10(1) na (2) ya Usajili, Uorodheshaji na Utoaji Leseni (**Registration, Enrollment and Licencing Regulation, 2010**).

Ofisi ya Msajili inawasisitiza Wauguzi na Wakunga wote ambao bado hawajakamilisha zoezi la kuhuisha Leseni kukamilisha taratibu zote ili kuepuka usumbufu usiokuwa wa lazima.

Kwa mawasiliano zaidi tafadhali piga simu na: - +255 787 951 966, +255 682 896 529, +255 628 583 890 na +255 758 589 706.

Nawatachia utekelezaji mwema.

Imetolewa na:



Agnes Mtawa

MSAJILI

BARAZA LA UUGUZI NA UKUNGA TANZANIA

26. 09. 2023